# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 045 SEPTEMBA 2024

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 MHE. MWIGULU: SERIKALI ITAENDELEA KUIPA KIPAUMBELE TMA

## 2 TMA YAWAKUMBUSHA WAHANDISI KUZINGATIA HUDUMA ZA HALI YA HEWA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI




## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2024



## KITAIFA

# MHE. MWIGULU: SERIKALI ITAENDELEA KUIPA KIPAUMBELE TMA

**Arusha**




Waziri wa Fedha, Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba aliipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kuahidi kuwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha itaendelea kuipa kipaumbele kwa kuwa huduma za hali ya hewa zinasaidia katika mipango mbalimbali ya maendeleo.

"Wataalam wa hali ya hewa mnafanya kazi nzuri, utabiri unaotolewa hivi sasa ni wa usahihi na umesaidia sana katika masuala ya kiuchumi na kijamii na mipango ya nchi kwa ujumla". Alizungumza Dkt. Mwigulu alipotembelea banda la TMA katika viwanja vya AICC, Arusha wakati akifunga rasmi Jukwaa la 16 la Ununuzi la Afrika Mashariki.



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitoa elimu kwa wadau mbalimbali wa Ununuzi kuhusu matumizi sahihi ya huduma za hali ya hewa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi nchini.

Hayo yalizungumzwa na Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dkt. Hamza Kabelwa katika mada aliyoiwasilisha akieleza kuwa, kiasi kikubwa cha matumizi ya fedha kinahusisha ununuzi, ni vyema huduma za hali ya hewa zikapewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mipango ya ununuzi na miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ili kuongeza thamani ya fedha katika mradi.

“Kwa kipindi cha hivi karibuni tumeshuhudia miradi mingi ikisimama kutokana na madhara yatokanayo na hali mbaya ya hewa, ni muda muafaka sasa wadau wanaohusika kuhakikisha wanatumia huduma hizo wakati wa ubunifu na kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi yao”. Alisisitiza Dkt. Kabelwa.



Katika hatua nyingine, wataalaam kutoka TMA kupitia maonesho yanayoendelea katika viwanja vya AICC, walieleza pia huduma za hali ya hewa zinahitaji uwekezaji wa miundombinu ya kisasa na gharama kubwa za uendeshaji ili kuwezesha utoaji wa huduma bora, hivyo ni vyema kwa wadau mbalimbali kujitokeza kutumia huduma hizo sambamba na kuchangia gharama kidogo ya huduma mahsusi.





JARIDA LA MWEZI

05 TOLEO NA. 045 SEPTEMBA 2024

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# TMA YAWAKUMBUSHA WAHANDISI KUZINGATIA HUDUMA ZA HALI YA HEWA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI

**Dar es Salaam**



Wahandisi nchini wamekumbushwa umuhimu wa huduma za hali ya hewa sambamba na kuchangia gharama za upatikanaji wa huduma hiyo katika utekelezaji wa miradi yao. Hayo yalizungumzwa na Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dkt. Hamza Kabelwa katika mada iliyowasilishwa katika Mkutano wa 21 wa Wahandisi uliyojumuisha wahandisi wa ndani na nje ya nchi katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, tarehe 05 hadi 06 Sepetemba, 2024.

Dkt. Kabelwa alieleza kuwa, katika hotuba ya Waziri wa Fedha ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25, kifungu cha 158 ilijumuisha mapendekezo ya mabadiliko ya kufanya marekebisho ya sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, sura 157 kuhusu Ada za Hali ya hewa kwa usalama wa uendeshaji wa miradi ya ujenzi. "Lengo la hatua hiyo ni kuongeza mapato yatakayowezesha utoaji wa huduma mahsusi za hali ya hewa ili kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kazi na kuimarisha usalama wa watu na mali katika maeneo ya miradi ya ujenzi, ambapo mchakato wa upatikanaji wa huduma hizo unahitaji uwekezaji wa miundombinu ya kisasa na gharama kubwa za uendeshaji". Alifafanua Dkt. Kabelwa.

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2024


Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2024, mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, mvua za chini ya wastani hadi wastani pamoja na mtawanyiko hafifu zinatarajiwa katika maeneo mengi. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi hadi joto kali inatarajiwa hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua. Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya pili.** |
| **Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kati ya wiki ya tatu na ya nne.** |
| **Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** | ♦ Vipindi vya mvua inayoambatana na ngurumo za radi vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.** |
| **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Oktoba,2024. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kuelekea mwishoni mwa mwezi.** |
| **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** | ♦ Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinaweza kujitokeza katika maeneo machache.** |
| **Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** | ♦ Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua na hali ya baridi kiasi inatarajiwa katika maeneo ya miinuko.** |
| **Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** | ♦ Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa kujitokeza wiki ya nne ya mwezi.** |
| **Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma):** | ♦ Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya miinuko.** |

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO SEKTA YA HALI YA HEWA

## Vifaa vya hali ya hewa visivyotumia zebaki

Mamlaka imefanikiwa kutekeleza matakwa ya kimataifa ya uondoshaji wa vifaa vinavyotumia zebaki katika shughuli za uangazi kwa asilimia 100 kwa vituo vikuu vya uangazi. Baadhi ya vifaa hivyo ni vifaa vya kupima joto la hewa na mgandamizo wa hewa visivyotumia zebaki (temperature transmitter and barometric pressure) vilivyofungwa katika vituo mbalimbali vya hali ya hewa nchini.



*Kifaa kinachotumia zebaki katika shughuli za uangazi.*




*Kifaa kisichotumia zebaki katika shughuli za uangazi.*


JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 044
AGOSTI 2024
TMA
1 WADAU WAHIMIZWA KUTOA MAONI YAO NA KUTEKELEZA MAAZIMIO YA MKUTANO IPASAVYO
2 TANZANIA YAWANOA WATAALAMU WA HALI YA HEWA AFRIKA KUHUSU MATUMIZI YA RADA ZA HALI YA HEWA
3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2024


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa



www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.